BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Saba – Tarehe 27 Septemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Biashara na Viwanda ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Wizara ya Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Biashara na Viwanda ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

153. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Katika vipindi tofauti vya vikao vya Baraza, Mawaziri wenye dhamana za Wizara wanaziongoza waliahidi mambo mengi ya wanachi.

(a) Je ni Mawaziri wangapi waliofatilia ahadi hizo kwa kufuatilia “Hansard” zao kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa ahadi hizo.

(b) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa kushindwa kutekeleza ahadi zao wanazozitoa katika vikao mbali mbali ndani ya chombo hiki muhimu cha wananchi.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

102. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Pamoja na Mawakili kuchukuliwa kuwa ni maafisa wa Mahakama, bado maafisa hao wanakosa Ofisi za kufikia na kujiandaa kwenye kesi katika Mahakama Kuu na mahakama nyenginezo na kulazimika kusimama kwenye “corridor”. Aidha, baadhi ya wakati huondoshwa kwenye “corridor” hizo bila ya kupewa sehemu nyengine na kuleta usumbufu kwao na wateja wao ambao ni wananchi wetu.

(a) Je, hatua gani za haraka zitachukuliwa ili kuwapatia ofisi ya kufikia Mawakili wa Kujitegemea kama zinavyofanya mahakama nyingi za nchi za Jumuiya ya Madola ikiwemo Tanzania bara.

(b) Je, kwanini Uongozi wa Mahakama unawasumbua na kuwafukuza Mawakili hao wanapolazimika kusimama kwenye ‘corridor’ ili kusubiri kesi zao wakati hawajawapatia ofisi rasmi kama walivyopatiwa Mawakili wa Serikali.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

113. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Barabara ya Shungi Skuli kuelekea Misooni katika Jimbo la Chake Chake, imekuwa haipitiki katika kipindi cha mvua na hivyo kusababisha matatizo makubwa kwa wakaazi wa maeneo hayo ambapo karibu huduma zote za kijamii ni lazima wazifuate kwenye barabara ya shungi.

(a) Je, Serikali inalijua tatizo hilo la barabara hasa kipindi cha mvua.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuishughulikia barabara hiyo ipitike wakati wowote.

(c) Je, mpango huo utatekelezwa katika bajeti ya mwaka gani.

Wizara ya Fedha na Mipango:

67. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Lengo la Serikali la kuanzisha maeneo ya uwekezaji ni kuongeza kipato cha Taifa sambamba na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu. Hata hivyo wapo baadhi ya wawekezaji ambao wameshindwa kuyaendeleza maeneo hayo na badala yake wameyajengea kuta na kukosekana tija kwa Serikali na wananchi hasa kwa upande wa Pemba.

(a) Je, ni miradi mingapi ya ujenzi wa hoteli huko Kaskazini Pemba iliyopewa vibali kuanzia mwaka 2000 – 2017 ambayo imeshindwa kuendelezwa.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kufuta hati zote zilizotolewa kwa wawekezaji ambao wameshindwa kuyaendeleza maeneo waliyopewa kwa mujibu wa sheria.

125. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Mwaka wa fedha 2017/2018, miongoni mwa mipango ya Maendeleo ya Serikali ilikuwa ni kununua "Land Craft", sambamba na Mradi wa Serikali mtandao awamu ya pili, jambo ambalo lingeongeza ufanisi wa kazi na kuongeza mapato.

(a) Je, ni hatua gani imefikiwa katika ukamilishaji wa miradi hiyo.

(b) Je, miradi hiyo miwili iligharimu kiasi gani hadi kukamilika kwake.

(c) Kama miradi hiyo haijakamilika, ni lini itakamilika.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

110. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na jitihada za Serikali kuinua sekta ya elimu, bado kuna tatizo hasa katika lugha ya kiingereza, kutokana na lugha hiyo kufanywa kama somo tu badala ya kufanywa kuwa lugha ya kufundishia.

(a) Je, Serikali inaonaje kutumia lugha ya kiingereza kama lugha ya kufundishia katika maskuli badala ya kuwa ni somo tu hasa kutokana na umuhimu wake katika mikataba, vyombo vya sheria na mikutano ya Kimataifa.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa suala hili hasa kwa kuzingatia kuwa mfumo huo unatumiwa na skuli za binafsi kama moja ya silaha ya matokeo mazuri ya mitihani yao.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

49. MHESHIMIWA KHADIJA OMAR KIBANO (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa Serikali ilifanya uhakiki wa mashamba ya eka tatu.

Je, Serikali itawarejeshea wananchi wake yale mashamba ya eka tatu.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

13. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji

Bandari ya Zanzibar kwa muda mrefu imekuwa ikizidiwa na mizigo na kumekuwa na uchelewaji wa kutoa mizigo na meli nyegine kusubiri.

Je, kwanini Bandari ya Zanzibar haianzishi mpango wa kufanyakazi kwa saa 24 ili kupunguza mrundikano wa mizigo.

Wizara ya Afya:

15. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hospitali ya Abdalla Mzee ni Hospitali ya Mkoa kwa Pemba ambayo ndio sehemu ya kwanza kupokea rufaa kutoka vituo vyengine na Hospitali za Wilaya. Hata hivyo kazi za upasuaji zinazofanyika katika Hospitali hiyo karibu kila siku zinahitaji kuwepo kwa mitungi ya kutosha ya gesi hasa ukizingatia kuwa hakuna mtambo wa gesi.

Je, ni lini Hospitali ya Abdalla Mzee itajengewa mtambo wa gesi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

Ripoti ya Wizara ya Biashara na Viwanda ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Wizara ya Fedha na Mipango:

Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
27 Septemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.